MAHUBIRI N°15: AMBACHO MUNGU ANANGOJEA KWETU

(*Ilihubiriwa jumapili asubuhi, 01 june 2003 pa Locodjro, Abidjan - Côte d'Ivoire / www.matth25v6.org*)

…Wakati tunapo gundua Kweli isiyo weza kupingwa ambayo iliahidiwa kwa wakati wetu, kinacho baki kwetu ni kuipeleka popote mahali kunaweza kupatikana mtoto wa Mungu, awe maskini au tajiri, awe mbali au karibu. Mungu aliye mwenye haki hataruhusu tuingie paradiso pasipo kutuuliza damu yao. Kama utu wa binadamu ni takatifu kama inavyo semwa na sheria ya wanadamu, nafsi ni takatifu tena sana zaidi. Kazi kubwa inatulazimishwa. Jukumu ya Math.28:19 siyo kwa kartasi wala vitabu lakini kwa watu, ambao ni sisi! Kitabu hakitajibu swali! Munaona? Mungu alipoona kwamba uzao wa binadamu unaelekea wima kwa upotevu, akaacha ukuu wa uungu wake na utukufu wake wote kwa kujitoa kama zabihu kwa ajili yetu ili tuwe na uzima wa milele kama yeye. Kitu kubwa ambacho Mungu aliweza kumupa mwanadamu, ni uzima wake binafsi. Japo, anapo kaa katikati ya malaika, hangelishuka, angeli baki tu Mungu lakini akaifanya ili tuwe na uzima. Munaona? Ijapo ni nini watu wanaita sifa na inayo wazuia kujiweka kwa kazi ya Mungu? Sijui! Katika Math.4:8-9, Shetani alitaka kumupa Yesu yote lakini akaikataa! Ndio maana hatujiingizi katika siasa […]

Mtu anapojidai kumtumikia Mungu, tafuteni kujua asili ya mwito wake, kutumwa kwake na mamlaka yake kabla ya kutafuta kujua kama anachosema wala anachofanya ni kweli. Wakati Mungu hakumtuma mtu, hawezi kubali bidii hata mambo mema ya mtu huyo. Kuhubiri haki haisemi kitu kwani shetani yeye binafsi anajua Neno.

Mapenzi kamilifu ya Mungu ilikuwa kwamba nabii aongoze Israeli badala ya mfalme. Lakini Israeli akaomba mfalme, 1Sam.8:4-7. Mungu hasemi kupitia mfalme lakini kwa nabii. Mbele ya kufa kwa Samweli, alipaswa kumpaka mafuta nabii mmoja kwa nafasi yake. Na kama kuwekwa kwa mfalme aliye chaguliwa na nabii siyo mapenzi kamilifu ya Mungu basi siyo rais aliye chaguliwa na wanadamu ndiye atakayekuwa mapenzi kamilifu ya Mungu. Katika 2 Wafalme 22:11-14, mfalme Yosia akatuma kuhani Hilkiya na mwandishi Akhikam kwa nabii ili awajulishe Neno la Mungu linasema nini. Katika 2Sik.20:20, mfalme Yosafati akaambia Israeli: *"mwamini Bwana, Mungu wenu, hivi atawasimamisha ninyi imara; mwamini manabii wake, hivi mutasitawi".*

Mkristo ni kama askari ambaye ameitwa kukufa siku moja kwa ajili ya nchi yake, kama iwezekanavyo. Siku mwito unalia kwa kupita kwa ushambulizi, yote duniani haina faida hata moja, siyo tu pesa na nyumba yake ndivyo vinatolewa kwa hatari lakini alicho nacho ambacho ni cha damani sana, uzima wake. Ndio maana inawabidi kuwa tayari kwa mwito wa jemadari. Na hiyo siyo katika mwezi moja, wala mwaka moja lakini leo. Biblia na ono vinaihakikisha ndio maana katika ono la 1993, munaona mwana kondoo aliye mfano wa zabihu. Ile ono imetafsiriwa kwa jumla ila tu njiwa wawili ambao ni watu wawili walio na Roho ya Mungu wa kweli juu yao na watakao kuja tu kwa kuniambia jambo fulani. Sijui ni kwa wakati gani lakini nitajua kwamba wanakuja kutoka kwa Mungu kama vile nilivyo ona katika ono. Munaona?... Na kupatana na Matendo16:6-10, Roho mtakatifu ataongoza hii uamsho katika shamba la utumishi. Yote inapaswa kuingia katika mpango wa mapenzi yake kama sivyo ni zambi vile vile, na ninazani kwamba kama aliniita hapo alinijua kabla kuwekwa msingi dunia na alijua nguvu zangu. Alipo rudisha funguo za ufalme kwa Petro, alijua Petro ni nani! Namna gani ujumbe huu utafikia mipaka za dunia, anaijua na ni wale walio na ile imani kama ya Yoshua na Kalebu ndio watakao ingia. […].

Kitabu cha mchungaji mubatisti kitanipa nini isipokuwa tu kunifanya mubatisti mwema! Wakati usomi wa Biblia ulikatazwa na papa Innocent III, ni shabaha gani Shetani alipenda kufikia? Ni ile ile shabaha ameifikia leo kwa njia ingine, ili alete watu kutii mapenzi yake. Anapo acha Biblia mikononi mwao, amewapa umati wa tafsiri. Namna ya kibatisti, wapentekoste, mashahidi wa Yehova, waadventisti, wanaziri,… anafikia kabisa kwa ukamilifu ile ile shabaha ; mtoto wa Mungu anaye husika na Wokovu pamoja na uzima wa milele, atatafuta hata kwa nukta ndogo ndogo ili ajue ukristo ni nini. Panya haiwezi kufugwa, mwana wa Shetani hata akikutana Kweli atabaki kile alicho. Mwana wa Mungu akikutana na uwongo atajiswali mpaka apate mwangaza! Amina! Munaona? Kilindi inaita kilindi.

Kati ya mwaka 1540 hata 1570, wakristo milioni tisa wakachomwa wakiwa hai, wakazikwa hai, wakakatwa vichwa,… hapana kwa Roma ya upagani lakini kwa Kanisa katolika ya Roma. Sababu gani? … kwa mwaka 1415, Jean Huss, mkuu wa chuo kikuu cha Prague, akachomwa hai juu ya kuni! Sababu gani?... kwa mwaka 1384, John Wyclif, mwalimu huko Oxford akachomwa hai juu ya kuni! Sababu gani ?... mahakama ya eklezia iliyo wekwa kisheria na kanisa Katolika kwa mwaka 1229 ilimaliza kabisa wakaaji wa Albi. Sababu gani?... kwa aogusti 1572, katika usiku moja tu, wakristo 70000 wakauawa huko Paris na katika wilaya. Sababu gani?... KWA SABABU WALIPINGA ILE MUNAYOITA KANISA KATIKA SIKU HIZI! Walipinga mababu za kardinali Agré, wachungaji waheshimiwa Dion Robert, Benjamin Boni, Kpan René, Jean-Baptiste Nielbien, Paul Ayoh, André Kouadio,.. hao mashetani wanao nuka zambi na makosa, malaika walioangushwa, walio poromoshwa toka mbinguni na ambao hukumu haichoki kulia juu yao, wakidanganya wale ambao majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha Mwana Kondoo kabla kuwekwa msingi wa dunia. Wale Wasio jua kwamba kazi ya Mungu ni kukubali na kusikiliza yule aliye tumwa naye, Yoane 6:28-29.

Nilifanya utafiti juu ya kila mtume, nukta juu ya nukta na sasa ijapokuwa walisambazwa, walipigania mafundisho moja. Nyuma yao, wafwasi wao walishika yale yale mafundisho mpaka mateso ilipo wachukua… Hauwezi kudanganya mtoto wa Mungu! Na watu wanafikia hata kusema kwamba yale maroho wanao tenda katika yale makanisa ya kibatisti, kusanyiko za miungu, pentekoste, na zingine ni Roho-Mtakatifu! Ni makufuru! Ukizania kwamba roho inayotenda juu ya Kacou Gem, J-M. Domoraud,… Osborn, Morris Cerullo, ni Roho-Mtakatifu, ni vipi kwa ile inayo tenda juu ya mganga mchawi Zérédji au kuhani Abekan? Sitaki watoto wa Mungu walale pamoja na wale ambao hawakuzaliwa kwa kutubu. Munapoona foursquare, kanisa la zamani la tangu 1922, ikiwa kwa jumla katika FECI na katika CNEPE-CI. Wanabatiza kwa jina la Yesu-Kristo na pia kwa ubatizo ya utatu mtakatifu kwa jumla. Nendeni kule kuona udanganyifu na uchafu wa dunia, mtoto wa Mungu atakwenda kule kufanya nini? Kanisa, kwa kutazama kuingizwa kwake katika Matendo ya mitume na kuendelea kwake katika historia halina ujamii pamoja na ile munayoita leo "kanisa". Ni rahisi sana kubandika mwili ya ubatisti kwa kichwa hiki na kudanganya nayo mtoto wa Mungu? Hautaweza kubandika picha ya mwanamke juu ya kitambulisho na kuaminisha mtoto: "Ni mama yako!"

Atachunguza majina, kimo, rangi, umri,… Na ni rahisi! Ni ile ndio shetani anajaribu kufanya. Makanisa mengi lakini Biblia inasema kwamba wateule hawata danganywa kamwe! Amina!

Ni kwa ajili ya mambo yote haya tunaitwa na Mungu katika shamba la kazi! Sababu gani? Kwa kuzuia udanganyifu na kufunua shetani na ujanja wake. Uhakika na ukuu ya mwito wa Mungu unapiga kwa kila mkristo mwanamke na mwanamume. Kama mitume ni baba zenu na munajidai ya kuwa munatembea juu ya nyayo zao, halafu, pokeeni wito huu kama sauti inayo vuma ndani ya mioyo zenu, hata inapo kuwa ngumu. Mungu hawaite tena katika nyumba lakini katika shamba la utumishi. Ni wakati Kweli inapaswa kwenda mji kwa mji, kijiji kwa kijiji, kampeni kwa kampeni! ...kwa wagonjwa, kwa maskini, kwa matajiri, kwa vilema. Musirudi tena ndani ya nyumba za damani kwa pumziko lenu lakini katika nyumba ndogo ndogo mahali hamufikiri kwamba mutapata hata ndizi ya kuchoma kama chakula. Pamoja na nguvu mulio nayo katika kijiji hiki, nendeni katika kijiji ifwatayo! Musifanye hesabu! Mungu wa Elia aliye ongoza baba zetu mitume na wafwasi wao atawaongoza yeye mwenyewe.

Kwa mwaka 1415, Jean Huss, mkuu wa chuo kikuu akaacha kazi, akawa mfwasi wa muhubiri mdogo kwani alipata maandiko yake na nyuma alipoingia kilindi katika mafundisho, alikwenda mahali kwa mahali akihubiri kile ambacho watu waliita mafundisho inayo pingana na ile ijulikayo na wakubwa lakini ilio kuwa Kweli ambayo hakuna aliye weza kuipinga; hata alipochomwa hai. Tangu mitume hata Wesley, sikuona mtu wa Mungu kutia mpaka kwa huduma yake katikati ya kuta nne. *"Nendeni kote…"*. Hata iwe uwanja ya wakatholika, waislamu, wakiinjili, wanao abudu nyama, hubirieni popote! Hamuna la kuomba ruhusa kwa mtu yeyote. Ilikuwa namna hii kwa wahubiri wasujaa kwa muda wa miaka hizo 1900. Munaona? Watu wanajizania kwamba wao ni wakristo ijapo si wakristo. Ni ile tunalazimishwa kuwaambia kufwatana na Ezekieli 33:1-9 hata kama wanaiita hukumu. Hatuta bebeshwa mmenyuko wao. Mungu aliarifu Kaina akijua kwamba ataua Abeli. Katika Agano la kale, Mungu aliifanya kupitia manabii kwa bei ya damu yao. Kanisani, hakuifanya kupitia malaika wala kwa yeye mwenyewe lakini kupitia wakristo ambao ni sisi. Kwanza kupitia baba zetu mitume na wafwasi na sasa ni kupitia sisi. Basi siyo jambo mpya! Na ndio maana nawasihi musiweke mambo ya mwili mbele ya mambo ya roho! Wana wa shetani wanasumbukia kile watakuwa duniani, hata juu ya kujua maiti yao itakuwa namna gani nyuma yao, musiwaige! Kama munapaswa kuangaliwa kama mbwa na kwenda mbinguni, musirudi nyuma! Ikiwa munatarajia kwenda mbinguni na munakubali kwamba ni Mungu mwenyezi aliye sema nami tarehe 24 aprili 1993, pokeeni hii kama wito wa Bwana Yesu-Kristo mwenyewe. Mungu alijitoa kwetu na ni kwa hiyo pia anataka maisha yetu! Tufe kwa [maneno ya] ulimwengu na tuishi kwa [maneno ya] mbinguni! Kukopesha Mungu kile alicho tupatia, haipaswe kutazamiwa kama kujitoa sana!

Munaona? Na kama kusanyiko fulani haliongezeki,… sikose kusema kwamba, kwa ujumbe mpya, kama huu, kusanyiko moja, hasa katika mji, haliwezi pitisha miezi mitatu pasipo uongofu. Na mwenyi kubeba hii jukumu, ni kichwa. Na ikiendelea hivi, inamupasa kukubali kukaa kwa upole, yeye mwenyewe. Nitarudilia mambo haya.

Lakini, kwa waamini, kumbukeni mfano wa talanta na musiwe mitini zisiyo zaa matunda! Ndugu kama dada, kama mwanamke musamaria, fanyeni kwa namna watu wote wasikie ujumbe huu kando yenu… kama vile ndugu Bitty.

Pia, wote walio na mapato ya vitu wala pesa wanapaswa kutenda, wakiweka vitu vyao kwa kazi ya Mungu kama katika Ezdra 1:5-6.

Mungu awabariki, mkutano imekwisha. Nyumbani mwenu, musisahau kuniombea. Tunapo tengana kimwili, mungu atuchunge katika Roho moja hata tutakapo kutana tena.

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org